**102/3 KISWAHILI (*Fasihi*) (2018)**

**KCSE *Trial Exam*** ***MWONGOZO***

.

1. Mwongozo wa kusahihisha ushairi

a) Matibabu ya kiasili / Dawa za asili/dawa za Kisasa. (1x2) ala.2

b) kuonyesha kuwa dawa asili zinafaa kwa matibabu kuliko za Kisasa. Watu wazirejelee.al2

c) Ana matibabu ya kiasili

- Hosptiali kuna oparesheni ya visu ambayo anaogopa
- Kuna dawa za asili zisizopatikana hospitali. (3X1) ala 3.

d) umbo la shairi

- Beti Sita.
- Takhmisa/mishoro mitano.
- Mtiririko - vina vya ukwapi na utao vinafanana katika beti zote.-li,ni
- Mathnawi - vipande viwili.
- Mizani ni 8,8
- Lina kiisho - mshoro wa mwisho unarudiwa beti hadi beti katika beti zote. (6x1) ala.6

e) kupata idadi ya mizani inayotakikana

f) Haoni kile anachofuata kule hospitalini ili hali dawa zote zapatikana nyumbani. (1x1) al.1

g) Maana ya maneno kama yalivyotumiwa katika shairi. alama 4

i) Dhalili - Kudharauliwa,nyonge, maskini,dhaifu.

ii) Azali - zamani.

Sahali - Urahisi/ wepesi.

Tumbo nyangwe-tumbo lote

**RIWAYA**

2. a)

- Mnenaji ni Amani.
- Anamwambia Mtemi Nasaba Bora. (Hoja 2x1=2)

b)

- Balagha /mubalgha –kama huyu mwanangu basi mlizaa na nani?
- Methali –Pasi ya viganja viwili kofi hazilii. (Hoja 2x2=4: Lazima mtahiniwa athibitishe ndipo atuzwe alama 2 kwa kila hoja.mfano pekee wa tamathali:-alama 1)

c)

- Msemewa ni Mtemi Nasaba Bora.
- Kupenda ufahari au utukufu –alienzi kutambulika kuwa jabari au kiongozi wa pekee.
- Ukatili wake –anampuuza mbwa wake badala ya kumshughulikia kiafya;amri Amani wa Imani watume mbaroni wa kuzuiliwa :manaji n.k.
- Uendezaji wa kisasa-chuki yake dhidi ya nduguye mwalimu Majisifu.
- Ufuska /usherati-anajhusisha kimapenzi na Lowela hata mwanaharamu uhuru.
- Ufisadi –ananyakuwa afrdhi ya watu,namna aliyopata cheo cha utemi,kimapendeleo n.k.
- Mapuuza –uchafu katika mazingira yake,kuugua kwa Amani,vilio vya raia kupuuzwa.
- Uimla/udikteta –alifanya maamuzi yake bila kuwashiririkisha wanajamii.
- Matumizi mabaya ya cheo au mamlaka-anatumia utemi wake kuwadhulumu wanajamii mf:Amani kusingiziwa kwa babake motto uhuru.

- Wivu –anavyompiga Amani na kumtimua mkewe kwa kuwatuhumu kuwa wapenzi –eti aliwafumania.
- Utepetevu –hatekelezi majukumu ya nyumba au ndoa –mkewe Zuhura ni mpweke.
- Uhalifu –wizi wa ardhi n.k. (Hoja zozote 7x2=14)  20 marks

3.

- Kielezo bora cha uzalendo –wanafaa kuonyesha upendo kwa jamii kwa kujitoa mhanga kusaka haki mf:Amani na Imani Madhubuti.
- Uendelezaji wa harakati za ukombozi –kutoa mwelekeo wa kuzingatiwa katika kuikomboa jamii.Amani na Imani wanaongoza wanasokomoko kufanikisha ukombozi wa kisiasa,kijamii na kiuchumi.
- Kuwazindua wanajamii-Amani na Imani wanabainisha maovu ya utawala wa Mtemi Nasaba Bora na mwalimu Majisifu hata kukawa na haya ya mapinduzi.
- Kuendeleza vipawa –Amani anaendeleza kipawa cha utunzi/uandishi (mswada wake wa riwaya Kidagaa Kimemwozea.
- Kujitegemea katika maisha –vijana wa Sokomoko hata wageni wanatafuta ajira ili kujiruzuku mf:Amani ,Imani ,D.J n.k.
- Kubadili mitazamo hasi na finyu-Imani anabadili mtazamo wa wanajamii kwa kukiuka mwiko au marufuku ya kunywa maji yam to Kiberenge;mtazamo kuhusu watoto wenye kasoro n.k.
- Kudumisha maadili ya jamii/heshima-Amani na Imani wanakaa pamoja bila kuvunjiana heshima.
- Kuwajali na kuwahurumia wengine-Amani anakubali kukilea kitoto Uhuru,Imani anawatunza watoto wa mwalimu Majisifu licha ya ulemavu wao.
- Kielezo cha ukakamavu-Amani na Imani wanajitosa katika uwanja wa ukombozi wenye changamoto nyingi;wanavyokabiliwa na waovu kama Mtemi Nasaba Bora.
- Kielezo cha maridhiano/msamaha- Amani anamsamehe Mtemi Nasaba Bora kwa maovu aliyomtendea.
- Kuwa na maono- DJ anatabiri kupanda vyeo kwa Amani na Imani na wanatokea kuwa ….
- Kuendeleza utangamano wa wanajamii-Amani na Imani wanvyoshirikiana licha ya asili na malengo tofauti;Amani na madhubuti kuwa uhuru katika elimu/kupevuka kiakademiaAmani,Madhubuti n.k (Hoja zozote 10x2=20)

TAMTHILIA - KIGOGO

**4.**

**a)** "Mataifa mengi ya Afrika yamekumbwa na tatizo la uongozi mbaya." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya kigogo. (al 20)

Viongozi huangaisha wanyonge,Ashua anasema, "...na kuhangaishwa na wenye nguvu ndio hewa tunayopumua huko." (uk 2)

Wachochole hutumikizwa na viongozi, Kombe, Boza na Sudi wanafanya kazi ya kuchonga vinyago vya mashujaa kwa ajili ya sherehe za uhuru.

Viongozi hawajawajibika, kazi yao ni kukusanya tu kodi.Ni jukumu la viongozi kuhakikisha kuwa soko ni safi lakini hawajawajibika kulisafisha. Licha ya wananchi kutoa kodi,soko ni chafu.(uk 2)

Viongozi kutangaza kipindi kirefu cha kusheherekea  uhuru ni ishara ya uongozi mbaya.Mashujaa wanaenziwa kwa kipindi kirefu ilhali mambo ya kimsingi hayajazingatiwa.Wanasagamoyo wana matakwa mengi kuliko kipindi kirefu cha kusherehekea uhuru.

Majoka anafadhili mradi usio na msingi wa kuchonga vinyago huku watu wakiwa na njaa na wao ndio watalipia mradi huo.

Viongozi hushawishi wananchi kwa ahadi ili wawaunge mkono.Sudi anashawishiwa na Kenga kuchonga kinyago ili apate malipo mazuri;kuwa mradi huo utabadilisha maisha yake na jina lake lishamiri. Pia atapata tuzo nyingi na likizo ya mwezi mzima ughaibuni na familia yake (uk 11)

Aidha viongozi hutumia zawadi kufumba wananchi kuwa wanawajali na kujali hali zao.Kenga anawaletea Sudi, Boza na kombe keki ya uhuru.
Kulingana na Sudi, hayo ni makombo na keki kubwa imeliwa kwingineko.

Viongozi hawalindi usalama wa wananchi,wananchi wanaishi kwa hofu. Ashua anahofia usalama wao kuwa huenda wakashambuliwa.(uk 15)

Migomo inayotokea Sagamoyo na maandamani ni kwa sababu ya uongozi mbaya.Wauguzi wanagoma na pia walimu wakidai haki zao.Wafanyakazi wananyanyaswa.

Majoka hajali maslahi ya wanasagamoyo.Anafunga soko ambalo wananchi wanategemea na kupandisha bei ya chakula.Uchumi Sagamoyo unasorota kutokana na soko kufungwa, watu hawana mahali pa kuuzia bidhaa zao.

Majoka anafungulia biashara ya ukataji miti bila kujali hali ya anga Sagamoyo,hasara ni kwa maskinii, viongozi wamejichimbia visima.Mito na maziwa yanakauka na mvua isiponyesha, hata maji ya kunywa yatatoka ng`ambo.

Majoka hajali kuhusu kifo cha Ngurumo licha ya kuwa mfuasi wake.Anaagiza Ngurumo azikwe kabla ya jua kutua (uk 69)

Viongozi hupanga njama ilikuangamiza wapinzani wao;

a) Majoka na Kenga wanapanga njama ya kumtia Ashua ndani.Wanapanga aitwe ofisini mwa Majoka kisha Husda aitwe ili wafumaniane.Ashua anazingiziwa kuzua sogo katika ofisi ya serikali na kutiwa ndani.Husda anafunguliwa baada ya nusu saa.

b) Kifo cha Jabali kilipangwa.Jabali alikuwa mpinzani wa Majoka mwenye wafuasi wengi. Akapangiwa ajali barabarani kisha wafuasi wake wakazimwa na kumfuata jongomeo,chama chake cha mwenge kilimfuata ahera.

c) Tunu anapanga kufanya uchunguzi kuhusu chanzo cha ajali ya Jabali. Majoka anapopata habari hizi,anapanga kuzima uchunguzi huo.

d) Kenga na Majoka wanapanga kuondoa chatu mmoja. Chatu hapa wanarejelea Sudi au Tunu kwa kuwa ndio wanaoongoza mapinduzi. Wanahofia kutolewa uongozini na ili kuzuia hali hii, wanapanga kumwondoa mmoja wao.

"...chatu mmoja atolewe kafara ili watu wajue usalama upo,wakereketwa waachwe katika hali ya taharuki"

e) Majoka anapanga njama Tunu auliwe,anaumizwa mfupa wa muundi nia yake ikiwa ni kumkomesha asimpinge. Majoka anatumia polisi wake kutekeleza ukatili huo.

Katika hotuba ya Tunu anayowahutubia waandamanaji,Sagamoyo kuna uongozi mbaya.Anasema kuwa;

- pesa za kusafisha soko zimefujwa,
- soko linafungwa badala ya kusafishwa,
- haki za wauzaji zimekiukwa.

Viongozi hawasikilizi matakwa ya wananchi.Majoka hana wakati wa kuwasikiliza waandamanaji.Hataki kujua chanzo cha maandamano wala suluhu lake.

Majoka anadhibiti vyombo vya habari Sagamoyo, habari zinazopeperushwa katika runinga ya Mzalendo na picha za watu wengi sokoni wakiongozwa na Tunu zinamfanya Majoka kufunga runinga hiyo ya mzalendo.

Viongozi hutumia vitisho.Majoka anatishia Chopi kumwaga unga wake kwa vile polisi hawakuwatawanya waandamanaji,wanasagamoyo wanatishiwa kuhama Sagamoyo kwa juwa sio kwao,wanarushiwa vijikaratasi. (uk 52)

Majoka anatumia askari kutawanya raia badala ya kulinda uhuru wao.

Viongozi ni waongo.Majoka anatumia uongo ili kumteka Tunu.Anamhaidi jambo la kifahari, kumwoza Ngao Junior akirudi kutoka ng`ambo.

viongozi hutendea wananchi ukatili,watu wanaotiwa jela huchapwa na haki zao hukiukwa.Ashua ana majeraha kutokana na kichapo.

Viongozi hupanga uvamizi, Sudi anavamiwa (uk 54)

Viongozi wamekiuka sheria.Mamapima anadai kuwa anauza pombe haramu kwa kibali kutoka serikali ya Majoka.Ni hatia kuuza pombe haramu lakini viongozi huvunja sheria na kuwapa wauzaji kibali. (uk 61)

Sagamoyo hata viongozi hawafuati katiba.

> "...huku ni Sagamoyo, serikali na katiba ni mambo mawili tofauti." (uk 61)

Uongozi wa Majoka una ubaguzi, unafaudi wachache tu, wanaomuunga mkono.Asiya bibiye Boza anapata mradi wa kuoka keki mwa vile anauunga uongozi wa Majoka Mkono.

Viongozi hujulimbikizia mali. Kuna hoteli ya kifahari Sagamoyo,Majoka and Majoka modern resort.
Viongozi ni wanafiki.Majoka amepanga kuficha maovu yake mbele ya wageni.Ukumbi unapambwa na kurembeshwa huku kukiwa na maovu mengi Sagamoyo.Kuna mauaji, unyakuzi, njaa,maziara yamejaa Sagamoyo.

**FASIHI SIMULIZI**

**5.** -Hurafa (alama 1)
Ameshirikisha wanyama kama wahusika (alama 1)
- Usuli
- Unaeleza chanzo cha fisi_kuchechemea (alama 1)

(a) (i) Methali - Leo ni leo

(i) Semi

- Kumpasulia mbarika
- Kuvunjia heshima
- Wasio na mbele wala nyuma
- Amejaa tele mfukoni.

*Kutaja 1* *Mfano 1* *Zozote 2 x 2 = 4*

(b)

- Mwenye majitapo
- Mwenye nguvu
- Mwenye uwezo mkubwa
- Mdhalimu
- Mnyanyasaji
- Mjeuri *Zozote 5 x 1 = 5*

(c)

- Ndovu ni mwenye nguvu
- Anamdhulumu fisi kwa kutomlipa pesa baada ya kufanya kazi shambani.
- Fisi hana nguvu / mnyonge
- Fisi wanapoamua kuitisha haki wanapigwa mijeledi na waliosalia kuchechemea kwao.

*Hoja 4 x 1 = 4*

(d)

- Kuelimisha
- Kuburudisha
- Kuendeleza maadili *Hoja 3 x 1 = 3*

**6.**

- Ina gharama ya chini zaidi katika ukusanyaji wa data.
- Mtafiti anaweza kufikia idadi kubwa ya watu kwa kipindi kifupi.
- Inaweza kutumiwa katika mahijiano kama mwongozo kufidia udhaifu wa mhojiwa.
- Humpa mhojiwa muda wa kuwazia maswali na kufanyia uchunguzi kabla ya kuyajibu.
- Hojaji aghalabu hazina athari ya mtafiti kwa kuwa hujazwa kama hayupo.Habari za kweli hujazwa.
- Hija inaweza kudalishwa kulingana na kiwangao cha wajazaji au wahojiwa. (Hoja zozote **4x1=4)**

**b)**

- Gharama ya utafiti inaweza kuwa kubwa kiwango cha kutomudiwa na mtafiti.
- Mtazamo hasi wa wanajamii kuhusu hoja huenda ukwafanya wasijaze.
- Baadhi ya wanajamii wanaweza kumshuku mtafiti kuwa mpelelezi na wakakataa kutoa habari.
- Utafiti unaweza kukwamizwa kwa baadhi ya wahojiwa kudai malipo kabla ya kuhojiwa.
- Mbinu nyingine kama vile hojaji hujitaji wanaojua kusoma na kuandika.Wasiojua watakwamiza au wapotoshe matokeo.
- Vizingiti vya dini-Imani kwamba matendo ya fasihi simulizi ni ya kinyume cha imani yao.
- Kupotea au kufisidiwa kwa vifaa vya kuhifadhi data.
- Uchache wa wazee au wataalamu wa fasihi simulizi.
- Vikwazo vya watawala-huenda wakakataa kutoa idhini ya kufanya utafiti.
- Wadhamini ndo mara nyingi huamua mambo yanayochunguzwa,mahali pa kuchunguza na mawanda au upeo wa kuchunguza kwenyewe.
- Mtafiti huenda asiwe na wakati wa kutosha kuwahoji watu wengi.
- Matatizo ya uchukuzi na mawasiliano.
- Matatizo ya kibinafsi mf:mhoji kugeuka,mhojiwa,kutojua lugha ya wahojiwa n.k

- Ukosefu wa usalama.
- Tatizo kutafsiri data kutoka lugha za kijamii.(Hoja 8x2=16) 20 marks

HADITHI FUPI

TUMBO LISILOSHIBA WAHARIRI: ALIFA CHOKOCHO NA DUMU KAYANDA

Jadili ufaafu wa anwani TUMBO LISILOSHIBA kwenye hadithi hiyo.

Anwani ya Tumbo Lisiloshiba ni mwafaka kwa Hadithi kwa Hadithi fupi ya TUMBO LISILOSHIBA. Anwani hii imetumika kijazanda kuashiria ile hali ya kutotosheka na alichonacho binadamu. Mathalan, mtu anaweza kuwa na mali, rasilimali, cheo fulani na kadhalika; lakini akawa hatosheki kamwe, anataka aendelee kumiliki vitu zaidi na zaidi bila ya kuonyesha kuridhika kamwe. Anwani hii inadhihirika kwa jinsi zifuatazo;

Tumbo ni jitu halishibi kamwe. Jitu hili linakula vyakula vyote kwa hoteli ya Mzee Mago, lakini halishibi kamwe. Baadhi ya vyakula vinavyoliwa na jitu hili ni kama vile wali, nazi, mchuzi wa Nyama, Nyama ya kuchoma kwa mkaa, kachumbari, samaki wa kukaanga, chapati, kuku wa kukaanga, Mboga ya mchicha na kadhalika. Licha ya kula duru zaidi ya tano ya vyakula hivi, jitu hili halionekani kushiba kamwe.

Kudhihirisha kwamba jitu hili hajashiba, jitu lenyewe linamwahidi Mzee Mago kwamba litarudi katika mkahawa ule usiku inayofuata na linataka lipate chakula marudufu kushinda kile cha hivi leo. Kwa hakika, yanaonekana wazi kwamba tumbo la jitu hili halishibi kamwe.

Kadhalika, tumbo la wakubwa ambalo hapa limetumiwa kijazanda halishibi katika upande wa kujitaftia rasilimali zao. Licha ya viongozi hawa kuwa na mali na rasilimali kochokocho huwa wantaka wapate mali nyingine zaidi. Jitu na wenzake wakubwa wanataka wajemge majengo ya biashara na Starehe katika mtaa wa Madongoporomoka kwa kuwa hawajatosheka na mali waliyonayo.

Tumbo la viongozi halishibi katika unyakuzi wa ardhi za watu. Jitu na wakubwa wenzake wanataka kunyakuwa ardhi ya wanamadongoporomoka kwa sababu hawajatosheka na ardhi walinayo. Wanataka ardhi zaidi ya ujenzi wa majengo kama njia ya kupanua mji wao ambao hauna nafasi ya majengo zaidi.

Mji nao kiishara una tumbo lisiloshiba kutokana na majengo yaliyojengwa ya aina mbalimbali. Ingawa mji huu una majengo haya uanataka kupitia kwa wakubwa wake upate nafasi zaidi ya ujenzi ili kukidhia tumbo lake lisiloshiba. Nafasi hii itapatikana kutoka mtaa wa Madongoporomoka ambao uko karibu na mji huu. Wakubwa wanataka kuutwaa mji huu kwa minajili ya upanuzi zaidi.

Kupitia Sheria zilizoko tunaona hali ya kutotosheka ama kutoshiba kwa viongozi kisheria. Wakubwa hawa wanabadilisha Sheria kwa manufaa yao binafsi. Sheria hizi zzinanuiwa kumkandamiza mwananchi, ili akose nafasi ya kutetea haki yake ya kumiliki mali. Hii ndiyo sababu inayomfanya Mzee Mago kuwashauri wananchi wawatafute wanasheria waadilifu kama njia ya kupigania haki yao wasije wakapokonywa eneo la Madongoporomoka na viongozi.

Kwa kiwango kikubwa wateja wanaokuja mle mkahawani mwa Mzee Mago wanafanya hivyo kutokana na matumbo yao kutoshiba. Matumbo haya tayari yana njaa na ndipo wanakuja kuyataftia vyakulaa kutoka katika mkahawa huu. Jitu linapofika linawapata watu wakiwa tayari kuagiza vyakula kutoka katika mkahawa huu. Hata hivyo, jitu linaamua kuvinuanua vyakula hivyo vyote.

Wakazi wa Mdongoporomoka yanaonekana kushiba hali ya sahau, tumbo la akili la Mago halishibi sahau kamwe. Badala ya kusahau anaendelea kukumbuka mengi kuhusu jinsi ya kupigania haki, ili ardhi ya Madongoporomoka isichukuliwe na wakubwa walio na fedha Nyingi. Hii ni kutokana na uvumi ambao hauna nafasi zaidi ya upanuzi isipokuwa hii ya mtaa huu wa makabwela.